HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,
Baraza la Madiwani.

TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 19/05/2022

1.0. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka. Hivyo, taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya Mhe. Rais kupita Manispaa ya Ilemela na kusalimia Wananchi
ii. Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira
iii. Taarifa ya kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa
iv. Taarifa ya Ziara ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi
v. Taarifa ya chanjo ya ugonjwa wa polio kwa watoto chini ya miaka mitano
vi. Taarifa ya chanjo ya Uviko-19
vii. Taarifa ya Mtihani wa kidato cha sita mwaka 2022
viii. Taarifa ya Mtihani wa majaribio (Mock) kwa darasa la saba
ix. Taarifa ya ugawaji wa madawati, mifuko ya sementi na "computer" kutoka Ofisi ya Mhe; Mbunge.
x. Taarifa ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Buzuruga

Scanned with CamScanner

xi. Taarifa ya kukamilika na kuanza kutumika Zahanati za Masemele, Nyamadoke na Lumala.

xii. Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la Awali na la kwanza.

2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

i. **Mhe, Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 05/02/2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe,Samia Suluhu Hassan akiwa njiani kuelekea Bujora alipita katika Wilaya ya Ilemela eneo la Buzuruga na kuwasalimia Wananchi.

ii. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mwezi Machi 2022 Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira ilitembelea Manispaa ya Ilemela na ilienda kukagua upimaji wa Viwanja katika Mtaa wa Nyafla Kata ya Sangabuye.

iii. **Mhe, Mwenyekiti,** tarehe 23/03/2022, Halmashauri ilipokea Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) pamoja na mambo mengine, ilikagua miradi ya Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri na Stendi ya Mabasi na Malori Nyamhongolo.

iv. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo Mhe, Abdallah Ulega alifanya Ziara ya kikazi katika Manispaa ya Ilemela ambapo alikagua shughuli za uvuvi na ukarabati wa Miundombinu ya Mialo ya Kayenze na New Igombe.

v. **Mhe, Mwenyekiti,** Halmashauri inategemea kuanza zoezi la chanjo ya ugonjwa wa polio kwa watoto chini ya miaka 5 tarehe 18/05/2022 na kumalizika tarehe 21/05/2022. Chanjo itakuwa ni kwa njia ya matone na litatekelezwa na wataalam wetu kwa kutembea nyumba kwa nyumba. Matarajio ni kuchanja watoto 85,000 katika Manispaa ya Ilemela.

vi. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri inaendelea na zoezi la kuchanja Wananchi dhidi ya ugonjwa wa Uviko-19 ambapo lengo ni kuchanjwa Wanachi 181,000 hadi sasa jumla ya wananchi 81,000 sawa na asilimia 44.75 wamechanjwa. Wataalam wanaendelea kuwahimiza Wananchi wetu kuzingatia njia za kujikinga na ugonjwa huu ambazo ni za kawaida sana yaani kunawa mikono kwa sabuni, kuvaa barakoa, kuepuka mikusanyiko wa watu na kutumia vitakasa mikono.

Scanned with CamScanner

vii. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wanafunzi wa kidato cha sita wanaendelea na Mitihani yao ya mwisho ambayo ilianza tarehe 09/05/2022 na itamalizika tarehe 27/05/2022. Jumla ya Wanafunzi 768 wanafanya Mtihani huo me 238 na ke 530.

viii. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wanafunzi wa darasa la saba wanafanya Mtihani wa majaribio Mock kuanzia tarehe 18 – 19/05/2022 katika kuwaandaa na Mtihani wa Taifa. Mtihani huu hufanyika kila mwaka na jumla ya wanafunzi 13,172 wanashiriki.

ix. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo terehe 02/05/2022 Mhe, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk. Angelina Mabula kupitia Mfuko wa Jimbo alitoa vifaa vifuatavyo katika Mashule:-

- "computer"3 kwa Shule za Sekondari zilizofahaulisha zaidi ambazo ni Bwiru Boys, Kilimani na Nyasaka.
- Mifuko ya Sementi 150 kwa Shule 3 ambazo kila shule ilipata mifuko 50. Shule hizo ni Kangaye S/Msingi, Nyasaka Sek na Nyamhongolo Sekondari.
- Madawati 120 kwa Shule za Msingi Nyamadoke, Igombe, Pasiansi na Chasubi.
- Viti 90 na Meza 90 kwa Shule 22 za Sekondari.
- Sh.3,300,000/- ilipelekwa Tarura kwa ajili ya kufungua barabara mpya maeneo mbalimbali.
- Mifuko 600 ya Sementi kwa ajili ya uzalishaji wa tofali kwenda kwenye Taasisi ambazo ni Mashule na Sekta ya Afya.

x. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Buzuruga kwa ufadhili wa SEQUIP wa Sh.470,000,000 unaendelea vizuri na umefikia hatua ifuatayo:-

- vyumba 8 vya madarasa vimekamilika.
- Vyumba 3 vya maabara viko hatua ya umaliziaji
- Maktaba 1 iko hatua ya upauwaji
- Chumba 1 cha ICT kiko hatua upauwaji
- Matundu 20 ya vyoo me 10 na ke 10 hata ya umaliziaji
- Jengo la utawala liko hatua ya umaliziaji

xi. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ujenzi wa Zahanati za Masemele, Nyamadoke na Lumala zilizogharimu jumla ya Sh.392,812,872/- kutoka Serikali kuu, Halmashauri, Mhe, Mbunge na Nguvu za Wananchi zimekamilika na zinatoa huduma kwa wananchi.

Scanned with CamScanner

xii. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa katika kuandikisha watoto wa darasa la awali maoteo yalikuwa ni wanafunzi 7,602 walioandikishwa ni wanafunzi 7,160 sawa na asilimia 98.

Kwa upande wa darasa la kwanza maoteo yalikuwa kuandikisha wanafunzi 10,542 na walioandikishwa ni 12,472 na kuvuka lengo kwa asilimia 118.

Kwa upande wa Sekondari; tumepokea wanafunzi 10,714 me 5,328 ke 5,386 wa kidato cha kwanza na kuvuka lengo tulilopangiwa la kupokea wanafunzi 10,502 kwa asilimia 102.

Mheshimiwa Mweyekiti, naomba kuwasilisha.

Eng.Modest J.Apolinary

MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Scanned with CamScanner